# Ujumbe wa Krismasi

Watoto, Watoto hukusanyikeni karibu. Nina hadithi nzuri ya kuwaambia.

Miaka mingi iliyopita katika nchi ya Israeli mtoto mvulana wa kipekee sana alizaliwa.

Yosefu na Mariamu walikuwa wamesafiri mbali kufika Bethlehemu na walipofika huko, hawakuwa na mahali pa kukaa—hakukuwa na mtu ambaye angewakaribisha. Giza lilikuwa likiingia na bado hawakuwa na mahali pa kulala na mtoto alikaria kuzaliwa.

Yosefu, alipata mahali ambapo familia yake ingeweza kulala kwa usiku huo, haikuwa ya kupendeza hata kidogo, ilikuwa zizi chafu, penye harufu mbaya.

Hawakuogopa, kwa sababu walijua kwamba Mungu alikuwa pamoja nao. Mtoto ambaye Mariamu alikuwa amembeba alikuwa Mwana wa Mungu. Kupitia muujiza Mariamu kijana alipewa mwokozi wa ulimwengu kumbeba tumboni mwake. Kazi yake pamoja na ile ya Yosefu ilikuwa kumlinda na kumlea mtoto huyu wa pekee sana kwa ajili ya Mungu. Ikiwa Mungu alikuwa amewapa baraka hii, Mungu angewalinda na kuwaongoza mahali walipohitaji kuwa.

Hili ni somo ambalo sisi pia tunaweza kujifunza.

Mtoto huyu alikuwa Mfalme wa Israeli, lakini hakuzaliwa katika jumba la kifalme, alizaliwa zizini. Ng’ombe na kondoo walikuwa wa kwanza kumkaribisha mwana wa Mungu duniani.

Una maoni gani kuhusu hilo?

Mtu muhimu zaidi duniani alizaliwa na mifugo!

Alilelewa na mwanamume ambaye hakuwa baba yake halisi—lakini Yosefu alimpenda sana na alifanya yote aliyoweza ili kuona kwamba Yesu alitunzwa, kwa sababu Yosefu alimpenda Mungu sana na alikuwa mtu mwema.

Wakati mwingine Mungu hutupa mama na baba ambao sio mama na baba wa kweli watutunze na kutuonyesha njia za Bwana. Ni baraka ya ajabu iliyoje na tunaye Mungu wa ajabu.

Kwa hiyo, baada ya Yesu kuzaliwa, Yosefu akamvika katika kitambaa alichokuwa nacho na kumlaza horini. Kufumba na kufumbua, wageni wakaanza kuingia.

Je, alikuwa ni Kuhani Mkuu wa Israeli? Hapana

Je, alikuwa ni mfalme Herode wa Israeli? Hapana

Je, alikuwa ni liwali wa Bethlehemu? Hapana

Walikuwa ni kundi la wachunga kondoo wasiooga ambao walikuwa wakinuka kama kondoo waliokuwa wakilala nao.

Walikuwa wakiwachunga kondoo wao usiku—wakiwalinda dhidi ya mbwa-mwitu na wezi wanaopenda kuja usiku wakati kondoo hawana usalama zaidi. Kondoo hawa hawakufugwa zizini bali walikuwa nje kondeni. Hawa walikuwa kondoo maalum na wachungaji wa kipekee. Kondoo hawa walikuwa wa Hekalu la Mungu.

Yesu alipozaliwa, Malaika walikwenda kwanza kwa wachungaji, na kuwaambia Masihi, mwokozi wa Ulimwengu amezaliwa.

Mwanzoni, wachungaji waliogopa sana, lakini malaika aliwaambia wasiogope kwamba walikuwa na ujumbe wa ajabu kwao.

Ni heshima iliyoje! Ni baraka iliyoje!

Kisha malaika wote wakaanza kuimba, "Utukufu kwa Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia!"

Je, unaweza kuwaza namna kwaya ya malaika inavyosikika?

Wachungaji walikimbia haraka iwezekanavyo kumtafuta mtoto huyo. Kidokezo pekee walichopewa ni kwamba alikuwa kwenye hori. Lakini hori gani?

Lazima wangebisha hodi kwenye kila mlango, na kuamsha kila mtu wakimtafuta mtoto huyu, na mwishowe wakampata.

Taifa zima lilikuwa likimngojea Masihi kwa miaka mingi, na ni nani walio wa kwanza kukutana naye? Wachungaji. Wachungaji wa hali ya chini waliokaa kule nje usiku na mchana pamoja na kondoo. Ingawa walikuwa wanyenyekevu, pia walikuwa na ujasiri kama Mfalme Daudi wa kale, ambaye angeweza kupigana na mbwa-mwitu waliojaribu kuiba au kuumiza kondoo. Mmoja wa wafalme wakuu wa Israeli pia alikuwa mchungaji. Kwa kweli, baadhi ya mashujaa wakuu wa Biblia walikuwa wachungaji. Ibrahimu, Isaka, Yakobo. Mchungaji wa kwanza tunayesoma kumhusu katika maandiko alikuwa Habili—mwana wa Adamu.

Kwa hiyo, wachungaji waliwaamsha watu wengi wakiwaambia walikuwa wanamtafuta Mwokozi, Masihi—lakini ni wao tu ndio walipaswa kwenda mahali ambapo Mariamu na Yosefu walikuwa.

Je, unaweza kuwaza jinsi walivyosisimka! Walikuwa wa kwanza kumwona Mwokozi sio tu wa Israeli, bali pia wako na wangu! Mwokozi wa ulimwengu wote.

Ikiwa ungekuwa mmoja wa wale wachungaji waliosikia malaika wakiimba na kukutana na mwokozi—ungefanya nini? Unafikiri walifanya nini baada ya kuondoka?

Naam, nadhani walichangamka sana hivi kwamba waliambia jiji zima usiku kucha kwamba walimpata. ( Luka 2:20 )

Je, unafikiri mtu yeyote kutoka mjini alikuja kumtembelea Yesu kwenye hori aliposikia habari kutoka kwa wachungaji?

Hapana, hawakufanya hivyo.

Siku nane baadaye, Yesu aliletwa hekaluni kulingana na Sheria ya Musa. Naye mzee aitwaye Simeoni akawajia Yosefu na Mariamu, akamchukua Yesu kutoka kwao, akamtukuza Mungu na kutabiri ili wengine wapate kusikia.

“Bwana na Mola, mimi ni mtumishi wako mpendwa, na sasa naweza kufa na kuridhika, kwa kuwa ahadi yako kwangu imetimizwa. Kwa macho yangu mwenyewe nimeliona Neno lako, Mwokozi uliyemtuma ulimwenguni. Atakuwa utukufu kwa watu wako Israeli, na Nuru ya Ufunuo kwa watu wote kila mahali! ( Luka 2:29-32 )

Mara tu baada ya hayo Ana nabii mke, na mjane mzee, “akawaendea, akabubujika kwa sauti kuu ya sifa kwa Mungu kwa ajili ya yule mtoto. Na tangu siku hiyo na kuendelea aliambia kila mtu

katika Yerusalemu ambaye alikuwa akingojea ukombozi wao kwamba Masihi aliyetazamiwa amekuja!” ( Luka 2:38 )

Je, unafikiri kuna mtu yeyote aliyewajali Simeoni na Anna? Hapana.

Mwana wa Mungu alikuwa ulimwenguni na hakuna aliyejali.

Wakati fulani tunahisi upweke katika ulimwengu huu. Jipe moyo na ujue kuwa Mungu yu pamoja nawe siku zote na hatakuacha kamwe. Atawatuma malaika wake maalum kukuchunga. Haijalishi yale wengine wanafikiria, ya muhimu ni anayoyafikiria Mungu.

Watu watakukatisha tamaa, lakini Mungu hatakukatisha tamaa.

Mkumbuke Yesu unapokuwa na huzuni. Kumbuka kwamba hakuwa maarufu na si tajiri katika ulimwengu huu, lakini bado ni Mwana wa Mungu. Hazina yake ilikuwa mbinguni na huko ndiko tunakotaka hazina yetu pia.

Msifu Mungu na umtegemee. Anakupenda kuliko mtu mwingine yeyote.